Issue no: 01 | **Vol no:** 07 | **August** 2026: 75-84

Uhawilishaji wa Utamaduni na Mwachano wake katika Tafsiri ya Fasihi: Tathmini ya Athari katika *Maisha ya Siri na Hadithi Nyingine*

Masibo Simon [1]
Mosol Kandagor [2]
Samuel Obuchi [3]

(1.2.3) Moi University, Kenya.
Main author's email: Simonmasibo6@gmail.com

Article History
Received: **2026.06.08**
Accepted: **2026.07.11**
Published: **2026.08.04**

Cite this article in APA
Simon, M., Kandagor, M., & Obuchi, S. (2026). Uhawilishaji wa utamaduni na mwachano wake katika tafsiri ya fasihi: Tathmini ya athari katika *Maisha ya Siri na Hadithi Nyingine*. *Editon consortium journal of Kiswahili*, *7*(1), 75-84. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v7i1.734

Ikisiri
Makala hii inachunguza uhawilishaji wa utamaduni katika tafsiri ya fasihi na jinsi unavyoathiri maana na ujumbe wa matini kwa hadhira lengwa. Utafiti unalinganisha matini chanzi *Secret Lives and Other Stories* na tafsiri yake ya Kiswahili *Maisha ya Siri na Hadithi Nyingine*. Utafiti ulitumia mkabala wa kimaelezo na uchanganuzi wa matini, ambapo dondoo tano zilizochaguliwa kimakusudi kutoka hadithi mbili, *Mubenzi Tribesman* (*Mubenzi*) na *A Mercedes Funeral* (*Mazishi ya Benzi*), zilichambuliwa ili kubainisha uhawilishaji wa vipengele vya kitamaduni kama nahau, taswira, marejeleo ya kijamii na istilahi za kiimani. Matokeo yanaonyesha kuwa baadhi ya dhana na taswira za kitamaduni zilipitia mabadiliko ya maana au kupoteza athari yake kutokana na ukosefu wa visawe vya moja kwa moja. Aidha, matumizi ya mikakati ya uenyejishaji na ugenishaji yalichangia ama kupunguza uzito wa kitamaduni wa matini chanzi au kurahisisha uelewekaji kwa wasomaji wa Kiswahili. Pia, marejeleo ya kihisia na mamlaka ya kijamii yalirekebishwa ili kuendana na utamaduni lengwa, jambo lililosababisha mwachano wa kidhima na kubadilika kwa athari ya ujumbe. Makala inahitimisha kuwa tafsiri ya fasihi ni mchakato wa uundaji upya wa utamaduni, ambapo maamuzi ya mtafsiri yanaweza kuhifadhi au kubadilisha mguso wa kitamaduni wa matini chanzi. Utafiti unapendekeza watafsiri kudumisha uwiano kati ya uelewekaji wa ujumbe na uhifadhi wa vipengele muhimu vya utamaduni ili kupunguza mwachano wa maana.

Maneno Muhimu: Mwachano wa kitamaduni, tafsiri ya fasihi, uhawilishaji wa utamaduni, ulinganifu wa kidhima, utotafsirikaji.

Editon OPEN ACCESS

This article is distributed under the license of a Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License. It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines.

UTANGULIZI

Tafsiri ya fasihi imeelezwa na wataalamu wengi kama mchakato unaovuka mipaka ya lugha na kuingia katika uhamishaji wa utamaduni, maana na mitazamo ya jamii moja kwenda nyingine (Bassnett, 2014; Lefevere, 1992). Kwa mtazamo huu, tafsiri si tendo la kiisimu pekee bali ni tendo la kitamaduni linalohusisha uamuzi wa kimkakati kuhusu namna ya kuwasilisha vipengele vya maisha, imani, na maadili ya jamii fulani kwa hadhira yenye muktadha tofauti. Hivyo basi, kila tendo la tafsiri ya fasihi huwa pia ni tendo la "uwakilishi wa utamaduni," ambapo mtafsiri huchukua nafasi ya mpatanishi kati ya tamaduni mbili.

Hata hivyo, mchakato huu hukumbwa na changamoto kubwa inayojulikana kama 'utotafsirikaji' *untranslatability*—yaani hali ambapo baadhi ya vipengele vya lugha na utamaduni haviwezi kuhamishwa moja kwa moja bila kupoteza maana au athari yake ya awali (Catford, 1965; Baker, 2018). Vipengele kama vile nahau, tasfida, mila, majina ya kiutamaduni, na imani za kijamii mara nyingi hujikita katika mazingira maalum ya kitamaduni kiasi kwamba havina viwakilishi sahihi katika lugha lengwa. Katika hali kama hizi, mtafsiri hulazimika kufanya uchaguzi kati ya kudumisha uhalisia wa utamaduni chanzi au kurekebisha ujumbe ili ueleweke katika utamaduni lengwa—hatua ambayo inaweza kuathiri uhalisia wa matini asilia.

Ndani ya muktadha huu ndipo dhana ya mwachano wa kitamaduni inapojitokeza kwa nguvu. Mwachano wa kitamaduni katika tafsiri unarejelea hali ambapo vipengele vya utamaduni vinabadilishwa, kupotoshwa au kupotea kabisa katika mchakato wa uhawilishaji, na hivyo kusababisha tofauti kati ya uzoefu wa msomaji wa matini chanzi na ule wa msomaji wa matini lengwa (House, 2015; Venuti, 1995). Tofauti hii inaweza kujitokeza kwa njia mbalimbali, ikiwemo uondoaji wa maana ya kitamaduni, uingizaji wa mitazamo ya utamaduni lengwa, au uundaji upya wa taswira zinazotofautiana na zile za matini chanzi.

Kwa mujibu wa Venuti (1995), mtafsiri anaweza kuchagua kati ya mikakati miwili mikuu: 'uenyejishaji' (*domestication*), ambapo matini hubadilishwa ili iendane na utamaduni lengwa, na 'ugenishaji' (*foreignization*), ambapo vipengele vya utamaduni chanzi huhifadhiwa ili kudumisha uhalisia wake. Hata hivyo, kila mkakati una athari zake. Uenyejishaji unaweza kusababisha kupotea kwa utambulisho wa kitamaduni wa matini chanzi, ilhali uigenishaji unaweza kuifanya matini kuwa ngumu kueleweka kwa hadhira lengwa. Hali hii inaonyesha kuwa tafsiri ya fasihi ni zoezi la kusawazisha mahitaji yanayokinzana—uaminifu kwa matini chanzi na uelewekaji kwa msomaji lengwa.

Tatizo kuu linalochunguzwa katika makala hii linahusu namna uhawilishaji wa vipengele vya utamaduni unavyochangia mwachano wa maana na athari katika tafsiri ya fasihi. Licha ya kuwepo kwa mchango mkubwa wa wataalamu katika taaluma ya tafsiri, tafiti nyingi zimejikita katika misingi ya jumla ya tafsiri na mikakati ya uhawilishaji wa maana kuliko uchunguzi wa kina wa vipengele vya utamaduni katika matini mahsusi za kifasihi. Kwa mfano, Newmark (1988) ameeleza tofauti kati ya tafsiri ya kisemantiki na tafsiri ya kimawasiliano, huku Baker (2018) akijadili changamoto za kutafuta visawe na kutafsiri nahau, misemo na vipashio vingine vya kiisimu. Vivyo hivyo, Venuti (1995) amejikita katika mjadala wa uenyejishaji na ugenishaji kama mikakati ya kuhawilisha utamaduni, ilhali House (2015) amesisitiza tathmini ya ubora wa tafsiri kwa kuzingatia ulinganifu wa matini. Ingawa tafiti hizi zimeweka msingi muhimu wa kinadharia kuhusu tafsiri na uhawilishaji wa utamaduni, hazijachunguza kwa kina namna vipengele mahususi vya utamaduni vinavyozalisha mwachano wa kitamaduni katika tafsiri ya hadithi fupi kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili.

Aidha, tafiti nyingi zinazohusu tafsiri katika muktadha wa Afrika zimejielekeza zaidi katika riwaya au masuala ya jumla ya tafsiri, huku uchanganuzi wa kina wa hadithi fupi ukibaki haba. Zaidi ya hayo, hakuna uchambuzi wa kina unaoonyesha jinsi mabadiliko ya vipengele vya kitamaduni yanavyoathiri upokeaji wa ujumbe kwa hadhira ya Kiswahili katika tafsiri ya *Secret Lives and Other Stories* na *Maisha ya Siri na Hadithi Nyingine*. Hivyo basi, makala hii inalenga kuziba pengo hilo kwa kuchunguza namna uhawilishaji wa utamaduni unavyozalisha mwachano wa kitamaduni na jinsi mwachano huo unavyoathiri maana na athari ya ujumbe katika tafsiri ya hadithi fupi kutoka Kiingereza hadi Kiswahili.

Kwa msingi huu, makala hii inalenga kuchunguza uhawilishaji wa utamaduni na mwachano wake katika tafsiri ya hadithi fupi, kwa kutumia matini chanzi *Secret Lives and Other Stories* na tafsiri yake ya Kiswahili *Maisha ya Siri na Hadithi Nyingine*. Lengo kuu ni kubainisha namna vipengele vya kitamaduni—kama vile

imani, taswira, lugha ya kijamii na mila—vinavyohawilishwa katika tafsiri, na jinsi mabadiliko hayo yanavyoathiri maana na athari ya ujumbe kwa hadhira ya Kiswahili. Aidha, makala inachunguza iwapo tafsiri hiyo imefanikiwa kudumisha ulinganifu wa kidhima au imezalisha mwachano wa kitamaduni unaobadilisha uzoefu wa msomaji.

Umuhimu wa utafiti huu uko katika nyanja kadhaa. Kwanza, unachangia katika taaluma ya tafsiri kwa kuonyesha kuwa tafsiri ya fasihi ni mchakato wa kitamaduni unaohitaji uelewa mpana wa jamii zote mbili—chanzi na lengwa. Pili, unatoa mwanga kuhusu changamoto ya 'utotafsirikaji' na namna inavyoathiri uhawilishaji wa maana katika tafsiri ya Kiswahili. Tatu, unatoa mchango wa kimatendo kwa watafsiri kwa kubainisha mikakati inayoweza kutumika kudumisha uhalisia wa kitamaduni bila kupoteza uelewekaji. Hatimaye, utafiti huu unapanua mjadala kuhusu nafasi ya tafsiri katika kuhifadhi au kubadilisha utamaduni, kwa kuonyesha kwamba tafsiri si daraja tu la kuvusha utamaduni bali pia ni chombo kinachoweza kuubadili, kuupunguza au hata kuufuta kabisa katika muktadha mpya.

MAPITIO YA MAANDISHI

Sehemu hii inakagua maandiko yanayohusiana na uhawilishaji wa utamaduni katika tafsiri ya fasihi kwa kulinganisha na kusintesia mitazamo ya wataalamu kuhusu nafasi ya utamaduni, changamoto za utotafsirikaji na mwelekeo wa tafiti zilizotangulia. Lengo si kurudia maelezo ya msingi yaliyotolewa katika utangulizi, bali kuonyesha maendeleo ya hoja za kitaaluma na kubainisha eneo ambalo bado halijachunguzwa kikamilifu.

Tafsiri na Utamaduni

Maandishi mengi yanakubaliana kuwa utamaduni ni sehemu isiyotenganishwa na tafsiri ya fasihi, lakini yanatofautiana kuhusu namna vipengele vya kitamaduni vinavyopaswa kuhawilishwa. Kwa mfano, Bassnett (2014) na Lefevere (1992) wanasisitiza kuwa maana ya matini haiwezi kueleweka nje ya muktadha wa kitamaduni unaoiunda. Kwa mtazamo wao, jukumu la mtafsiri ni kuhamisha mifumo ya maana na mitazamo ya kijamii badala ya kuhamisha miundo ya lugha pekee.

Ingawa wanakubaliana kuhusu umuhimu wa utamaduni, Lefevere (1992) anaona tafsiri kama uandikaji upya (*rewriting*) unaoathiriwa na nguvu za kiitikadi na kijamii zinazotawala utamaduni lengwa. Kinyume chake, Venuti (1995) anaelekeza mjadala katika uteuzi wa mkakati wa tafsiri kupitia uenyejishaji na ugenishaji. Kwa hiyo, wakati Lefevere anasisitiza mazingira ya kijamii yanayoathiri tafsiri, *Venuti* anasisitiza maamuzi ya mtafsiri kuhusu kiwango cha kuhifadhi au kubadilisha tofauti za kitamaduni.

Newmark (1988) anaunganisha mitazamo hii kwa kusisitiza kuwa mafanikio ya tafsiri hutegemea uwezo wa mtafsiri kusawazisha uaminifu kwa matini chanzi na uelewekaji katika lugha lengwa. Kwa hivyo, tofauti za mitazamo ya wataalamu hawa zinaonyesha kuwa changamoto kuu si iwapo utamaduni unapaswa kuhawilishwa, bali ni kiwango na namna ya kuuhawilisha bila kupoteza maana na athari ya matini.

Utotafsirikaji

Mjadala kuhusu utotafsirikaji unaonyesha kuwa si vipengele vyote vya lugha na utamaduni vinaweza kupata viwakilishi sawia katika lugha nyingine. Catford (1965) anatofautisha utotafsirikaji wa kiisimu na ule wa kitamaduni, akibainisha kuwa tofauti za kitamaduni ndizo chanzo kikuu cha matatizo mengi katika tafsiri ya fasihi.

Mtazamo huu unaungwa mkono na Baker (2018), ambaye anaonyesha kuwa nahau, methali, tasfida na marejeleo mengine ya kitamaduni mara nyingi hukosa visawe vya moja kwa moja. Hata hivyo, Baker anasisitiza matumizi ya mikakati ya kimuktadha kama ufafanuzi, ubadilishaji au urekebishaji ili kudumisha mawasiliano, ilhali Newmark (1988) anaonya kuwa mikakati hiyo inaweza kuhifadhi uelewekaji lakini ikabadilisha athari ya kisanii na kitamaduni ya matini chanzi. Hivyo, wataalamu hawa wanakubaliana kuhusu kuwepo kwa changamoto ya utotafsirikaji, lakini wanatofautiana kuhusu kiwango ambacho mabadiliko hayo yanapaswa kukubalika katika tafsiri ya fasihi.

Kwa hiyo, maandiko yaliyopo yanaonyesha kuwa utotafsirikaji si tatizo la ukosefu wa msamiati pekee, bali ni matokeo ya tofauti za kimfumo na kiutamaduni kati ya jamii zinazohusika katika tafsiri.

Tafiti Tangulizi

Tafiti zilizotangulia zimechangia kwa kiasi kikubwa kuelewa uhusiano kati ya tafsiri na utamaduni, lakini zimejikita katika maeneo tofauti ya uchunguzi. Nida (1964) alijenga msingi wa Nadharia ya Ulinganifu wa

Kidhima kwa kusisitiza umuhimu wa kuhifadhi athari ya ujumbe kwa msomaji wa lugha lengwa, ilhali Venuti (1995) alielekeza mjadala katika athari za mikakati ya uenyejishaji na ugenishaji kwa uwakilishi wa utamaduni. Kwa pamoja, tafiti hizi zinaonyesha kuwa uhawilishaji wa utamaduni ni suala la msingi katika tafsiri ya fasihi, ingawa hazitoi uchambuzi wa kina wa jinsi mikakati hiyo inavyojitokeza katika matini mahsusi.

Katika muktadha wa Afrika, Bandia (2008) anaonyesha kuwa tafsiri kati ya lugha za Kiafrika na lugha za kigeni hukumbwa na changamoto zinazotokana na tofauti za kijamii na kitamaduni. Hata hivyo, tafiti nyingi zimejikita katika riwaya au mijadala ya jumla ya tafsiri ya fasihi bila kuchunguza kwa kina namna vipengele mahususi vya utamaduni vinavyohawilishwa katika hadithi fupi. Aidha, tafiti hizo hazijaonyesha kwa kina athari za maamuzi ya mtafsiri kwa uzoefu wa msomaji wa lugha lengwa kupitia uchanganuzi linganishi wa matini.

Katika taaluma ya Kiswahili, hali hii inaonekana zaidi. Tafiti nyingi zimeelekeza nguvu katika nadharia za tafsiri au changamoto za jumla za uhawilishaji wa maana, huku zikiacha uchunguzi wa kina wa mwachano wa kitamaduni unaozalishwa na mikakati ya tafsiri katika matini mahsusi. Hivyo, bado kuna uhaba wa tafiti zinazochunguza kwa kutumia data za kimatini jinsi vipengele vya kitamaduni vinavyohifadhiwa, kubadilishwa au kupotea katika tafsiri ya hadithi fupi kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili.

Kwa msingi huo, makala hii inalenga kuziba pengo hilo kwa kufanya uchanganuzi linganishi wa *Secret Lives and Other Stories* na tafsiri yake *Maisha ya Siri na Hadithi Nyingine* ili kubainisha namna mikakati ya uhawilishaji wa utamaduni inavyozalisha mwachano wa kitamaduni na jinsi mwachano huo unavyoathiri uwasilishaji wa maana na uzoefu wa msomaji wa lugha lengwa.

Msingi wa Kinadharia

Makala hii inaongozwa na mikabala miwili ya kinadharia inayokamilishana katika uchanganuzi wa data, yaani Nadharia ya Ulinganifu ya Nida (1964) na mtazamo wa Uhawilishaji wa Kitamaduni wa Venuti (1995). Uchaguzi wa mikabala hii unatokana na ukweli kwamba utafiti huu haukusudia tu kutathmini iwapo tafsiri imefanikiwa kuwasilisha maana ya matini chanzi, bali pia ulilenga kuchunguza mikakati ya kitamaduni iliyotumiwa na mtafsiri na namna ilivyochangia kuhifadhi au kubadilisha vipengele vya utamaduni. Hivyo, Nadharia ya Ulinganifu ilitumika kama msingi wa kutathmini matokeo ya tafsiri, ilhali mtazamo wa Venuti ulitumika kueleza mikakati iliyozalisha matokeo hayo. Kwa pamoja, mikabala hii iliunda mfumo mmoja wa uchanganuzi uliowezesha kueleza si tu *kilichobadilika* katika tafsiri, bali pia *kwa nini* mabadiliko hayo yalitokea.

Nadharia ya Ulinganifu (Nida)

Kwa mujibu wa Nida (1964), tafsiri bora ni ile inayoweza kuwasilisha ujumbe wa matini chanzi kwa namna inayozalisha athari inayokaribiana kwa hadhira ya lugha lengwa. Nida anatofautisha aina mbili kuu za ulinganifu: ulinganifu wa kimuundo (*formal equivalence*) na ulinganifu wa kidhima (*dynamic equivalence*).

Ulinganifu wa kimuundo hulenga kuhifadhi muundo na vipengele vya kiisimu vya matini chanzi kadri inavyowezekana, ilhali ulinganifu wa kidhima hulenga kuhakikisha kuwa msomaji wa lugha lengwa anapata maana na athari inayofanana na ile ya msomaji wa matini chanzi. Katika tafsiri ya fasihi, ulinganifu wa kidhima hupewa uzito zaidi kwa sababu huzingatia uwasilishaji wa dhamira, hisia na athari za kisanii kuliko kufuata muundo wa lugha pekee.

Katika makala hii, Nadharia ya Ulinganifu ilitumika kama kigezo cha tathmini cha kuchunguza iwapo vipengele vya utamaduni vilivyohawilishwa katika *Maisha ya Siri na Hadithi Nyingine* vimedumisha maana, dhamira na athari iliyokusudiwa katika *Secret Lives and Other Stories*. Pale ambapo maana ya kitamaduni ilihifadhiwa, ilichukuliwa kuwa ulinganifu wa kidhima umefikiwa; na pale ambapo maana au athari ilibadilika, hali hiyo ilitafsiriwa kama mwachano wa kitamaduni.

Mtazamo wa Uhawilishaji wa Kitamaduni (Venuti)

Mtazamo wa Lawrence Venuti (1995) unasisitiza kuwa tafsiri ni tendo la kitamaduni linalohusisha maamuzi ya kimkakati kuhusu namna ya kushughulikia tofauti za kitamaduni kati ya matini chanzi na matini lengwa. Venuti anabainisha mikakati miwili mikuu: uenyejishaji na ugenishaji.

Uenyejishaji huhusisha kurekebisha vipengele vya matini chanzi ili viendane na matarajio na utamaduni wa hadhira lengwa, ilhali ugenishaji hulenga kuhifadhi upekee wa utamaduni chanzi hata kama baadhi ya vipengele vitabaki kuwa vya kigeni kwa msomaji wa lugha lengwa.

Kwa mujibu wa Venuti (1995), uchaguzi wa mkakati wowote kati ya hii miwili huathiri namna utamaduni unavyowasilishwa, kubadilishwa au kufichwa katika tafsiri.

Katika makala hii, mtazamo wa Venuti ulitumika kama kigezo cha kueleza sababu za mabadiliko yaliyobainika katika uchanganuzi. Kwa kila kipengele cha kitamaduni kilichochunguzwa, ilibainishwa iwapo mtafsiri alitumia mkakati wa uenyejishaji au ugenishaji, na jinsi uchaguzi huo ulivyoathiri uwasilishaji wa maana na utamaduni katika matini lengwa.

Muunganiko wa Mikabala Miwili katika Uchanganuzi

Katika utafiti huu, Nadharia ya Ulinganifu ya Nida na mtazamo wa Venuti havikutumika kwa kujitegemea, bali kama mikabala inayokamilishana katika hatua mbili za uchanganuzi. Kwanza, kwa kutumia Nida (1964), kila kipengele cha kitamaduni kilitathminiwa ili kubaini iwapo tafsiri ilifanikiwa kudumisha ulinganifu wa kidhima, yaani kuhifadhi maana, dhamira na athari ya matini chanzi kwa hadhira ya Kiswahili. Pili, pale ambapo mwachano wa kitamaduni ulionekana, mtazamo wa Venuti (1995) ulitumika kufafanua mkakati wa tafsiri uliosababisha mwachano huo, iwe ni uenyejishaji au ugenishaji.

Kwa hiyo, Nida alijibu swali la "nini kilitokea katika tafsiri?" kwa kupima kiwango cha ulinganifu wa maana na athari, ilhali Venuti alijibu swali la "kwa nini kilitokea?" kwa kueleza mikakati ya kitamaduni iliyotumiwa na mtafsiri. Muunganiko huu uliwezesha uchanganuzi usiishie kubainisha kuwepo kwa mwachano wa kitamaduni, bali pia kueleza chanzo chake na athari zake katika uwasilishaji wa maana kwa msomaji wa lugha lengwa.

Kwa msingi huo, makala hii inachunguza iwapo tafsiri ya *Maisha ya Siri na Hadithi Nyingine* imefanikiwa kudumisha ulinganifu wa kidhima huku ikihifadhi mguso wa utamaduni wa matini chanzi, au kama matumizi ya mikakati ya uenyejishaji na ugenishaji yamezalisha mwachano wa kitamaduni unaobadilisha maana na uzoefu wa msomaji.

MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulitumia muundo wa maktabani wenye mkabala wa kimaelezo. Mkabala huu ulifaa kwa kuwa uliwezesha uchunguzi wa kina wa vipengele vya lugha na utamaduni vinavyojitokeza katika matini teule bila kuhusisha ukusanyaji wa data za nyanjani. Kwa mujibu wa Creswell (2014), utafiti wa kimaelezo hulenga kufafanua na kueleza matukio au dhana kwa undani, jambo linalouwezesha uchambuzi wa kina wa maana na mitazamo iliyomo katika matini za kifasihi.

Data za utafiti zilipatikana kutoka matini mbili kuu: *Secret Lives and Other Stories* kama matini chanzi (MC) na tafsiri yake ya Kiswahili *Maisha ya Siri na Hadithi Nyingine* kama matini lengwa (MT). Matini hizi ziliteuliwa kwa kuwa zinatoa msingi mzuri wa kulinganisha namna vipengele vya utamaduni vinavyohawilishwa kutoka Kiingereza hadi Kiswahili, hasa katika muktadha wa hadithi fupi zenye msongamano wa maana na matumizi makubwa ya taswira za kijamii na kitamaduni.

Uteuzi wa data ulifanyika kwa kutumia mbinu ya usampulishaji wa kimakusudi. Kwa mujibu wa Patton (2002), usampulishaji wa kimakusudi humwezesha mtafiti kuchagua data mahsusi yenye uwezo mkubwa wa kujibu maswali ya utafiti. Katika utafiti huu, sampuli ilijumuisha dondoo tano zilizoteuliwa kutoka hadithi mbili, yaani *Mubenzi Tribesman* (*Mubenzi*) na *A Mercedes Funeral* (*Mazishi ya Benzi*), kati ya hadithi kumi na tatu zilizomo katika *Secret Lives and Other Stories* na tafsiri yake *Maisha ya Siri na Hadithi Nyingine*. Hadithi hizi ziliteuliwa kwa kuwa zilikuwa na idadi kubwa ya vipengele vya kitamaduni vinavyofaa kuchunguza uhawilishaji wa utamaduni katika tafsiri. Aidha, dondoo zilijumuishwa katika sampuli kwa kuzingatia vigezo mahsusi vya uwepo wa vipengele vya kitamaduni vinavyobeba maana muhimu katika matini, kama vile nahau, tasfida, marejeleo ya kidini, imani za kijamii, istilahi za kitamaduni na taswira zinazohusiana na maisha ya jamii. Vilevile, kila dondoo ilipaswa kuonyesha mabadiliko ya namna vipengele hivyo vilivyohawilishwa kutoka matini chanzi kwenda matini lengwa, hususan pale ambapo kulibainika uhifadhi, ubadilishaji au upotevu wa maana ya kitamaduni, jambo lililowezesha kuchunguza mwachano wa kitamaduni katika tafsiri.

Njia kuu ya uchanganuzi ilikuwa uchanganuzi wa matini, ambao ulihusisha kulinganisha moja kwa moja matini chanzi na matini lengwa ili kubainisha mabadiliko ya maana, mtindo na athari ya ujumbe. Kwa mujibu wa Munday (2016), uchanganuzi wa matini katika tafsiri unalenga kufichua namna vipengele vya lugha

vinavyobadilika katika mchakato wa uhawilishaji na athari zake kwa uelewa wa msomaji. Katika muktadha huu, uchanganuzi ulilenga hasa vipengele vya kitamaduni ili kubaini iwapo vilihifadhiwa, vilibadilishwa au vilipotea katika tafsiri.

Uchanganuzi wa data ulifanyika kwa hatua kadhaa. Kwanza, matini chanzi na matini lengwa zilisomwa kwa kina mara kadhaa ili kubaini vipengele vya kitamaduni vinavyojitokeza katika matini zote mbili. Pili, vipengele hivyo vilitengwa na kurekodiwa kwa kutumia jedwali la uchanganuzi lililoonyesha data ya matini chanzi, tafsiri yake katika matini lengwa na maelezo ya awali kuhusu mabadiliko yaliyobainika. Tatu, kila kipengele kilichanganuliwa kwa kulinganisha namna kilivyohawilishwa katika matini lengwa kwa kuzingatia Nadharia ya Ulinganifu ya Nida (1964) na mtazamo wa Uhawilishaji wa Kitamaduni wa Venuti (1995). Hatimaye, data ziliainishwa katika makundi ya kimaudhui kulingana na aina ya mwachano wa kitamaduni uliobainika ili kuwezesha mjadala wa matokeo.

Aidha, data zilizochaguliwa zililenga kuonyesha wazi mabadiliko ya vipengele vya kitamaduni katika tafsiri, kwa kutumia mifano mahsusi inayodhihirisha hali ya utotafsirikaji, uchujaji wa kitamaduni (*cultural filtering*) na uundaji upya wa maana. Kwa kufanya hivyo, utafiti uliweza kutoa msingi thabiti wa kuchunguza namna uhawilishaji wa utamaduni unavyoathiri ulinganifu wa kidhima na uzoefu wa msomaji wa lugha lengwa.

Uchambuzi wa data ulifanywa katika kipindi chote cha utafiti sambamba na usomaji wa matini teule, ambapo kila data iliyoteuliwa ilinakiliwa na kupewa nambari ya utambuzi ili kurahisisha urejeleaji wakati wa uchambuzi na mjadala wa matokeo. Ili kuhakikisha uaminifu wa uchambuzi, vigezo vya uteuzi na uchanganuzi wa data vilitumika kwa uthabiti katika mifano yote iliyochaguliwa. Aidha, uchambuzi ulirejelewa mara kadhaa kwa kulinganisha matini chanzi na matini lengwa ili kuthibitisha usahihi wa tafsiri na uthabiti wa hoja zilizotolewa. Kwa kuwa utafiti huu ulikuwa wa uchanganuzi wa matini uliofanywa na mtafiti mmoja, hakukufanyika uhakiki wa mfasiri mwingine (*inter-coder reliability*); badala yake, uaminifu wa uchanganuzi ulijengwa kupitia matumizi ya mfumo mmoja wa kinadharia, marejeleo ya moja kwa moja ya data za matini na ulinganishi wa kimfumo kati ya matini chanzi na matini lengwa.

Kwa jumla, mbinu hizi ziliwezesha uchanganuzi wa kina na wa kimfumo wa mwachano wa kitamaduni katika tafsiri, na hivyo kutoa majibu ya kuaminika kuhusu namna tafsiri inavyohusisha si tu uhamishaji wa lugha bali pia uundaji upya wa utamaduni.

MATOKEO YA UTAFITI

Sehemu hii inawasilisha uchanganuzi wa data teule ili kubainisha namna uhawilishaji wa utamaduni unavyochangia mwachano wa maana na athari ya ujumbe katika tafsiri ya *Maisha ya Siri na Hadithi Nyingine*, kwa kulinganisha matini chanzi na matini lengwa.

Majadiliano yamepangwa katika maeneo matano: uhawilishaji wa dhana za kitamaduni, mabadiliko ya taswira za kitamaduni, uchujaji wa utamaduni, changamoto ya utotafsirikaji na mikakati ya mfasiri, na athari kwa msomaji wa Kiswahili.

Kwa kuongozwa na Nadharia ya Ulinganifu na dhana ya uhawilishaji wa utamaduni, sehemu hii inaonyesha kuwa tafsiri si uhamishaji wa lugha pekee bali ni mchakato unaoweza kubadilisha uzoefu wa kitamaduni wa matini.

Uhawilishaji wa Dhana za Kitamaduni

Sehemu hii inachunguza namna dhana za kitamaduni zinavyohawilishwa katika tafsiri na jinsi mchakato huo unavyozalisha mwachano wa maana na athari ya ujumbe. Dhana za kitamaduni hapa zinarejelea vipengele vinavyobeba maana za kijamii, kiuchumi au kidini ambazo hueleweka kikamilifu ndani ya muktadha wa utamaduni fulani. Kama anavyoeleza Newmark (1988), vipengele vya aina hii mara nyingi hukosa visawe vya moja kwa moja katika lugha lengwa, na hivyo kumlazimu mfasiri kufanya maamuzi ya kimkakati ambayo yanaweza kuathiri ulinganifu wa kidhima.

Mfano wa kwanza unaonekana katika Data 1, ambapo kirai cha Kiingereza *“market days”* kimetafsiriwa kama *“siku za soko kukutana”*.

Data 1

MC: Market days - burst with people (uk. 122).

MT: Siku za soko kukutana, masoko yote yalifurika watu… (uk. 147).

Katika muktadha wa matini chanzi, “market days” ni dhana ya kijamii inayorejelea siku maalum za gulio zenye umuhimu wa kiuchumi na kijamii katika jamii husika. Hii si tu rejeleo la shughuli ya kibiashara, bali pia

tukio la kijamii lenye utaratibu maalum. Tafsiri ya *"siku za soko kukutana"* inapotosha dhana hii kwa kuhamisha mkazo kutoka kwenye tukio la kitamaduni hadi kitendo cha kukutana, jambo linalopunguza uzito wa maana iliyokusudiwa. Kwa mtazamo wa Nida (1964), hapa ulinganifu wa kidhima haujafikiwa kwa kuwa msomaji wa Kiswahili hapati athari ileile ya kijamii na kitamaduni inayopatikana katika matini chanzi. Vilevile, Data 2 inaonyesha changamoto ya uhawilishaji wa dhana za kidini na kiutamaduni.

Data 2

MC: Today <u>under the old sacred tree *Mugumo*</u> –
<u>a black ram</u>, without any blemish, <u>was sacrificed</u> (uk. 22).

MT: Leo, <u>chini ya ule mti mtakatifu *Mugumo*</u>, <u>beberu mweusi</u>,
asiyekuwa na kilema, <u>alitolewa kafara</u> (uk. 24).

Kirai *"under the old sacred tree Mugumo – a black ram… was sacrificed"* kimetafsiriwa kama *"chini ya ule mti mtakatifu Mugumo, beberu mweusi… alitolewa kafara"*. Hapa kuna mabadiliko mawili muhimu. Kwanza, kuachwa kwa kipengele cha *"old"* kunapunguza uzito wa kihistoria na kiutamaduni wa mti wa Mugumo, ambao katika baadhi ya jamii za Kiafrika huashiria uhusiano wa vizazi na ulimwengu wa kiroho. Pili, kubadilishwa kwa *"ram"* kuwa *"beberu"* kunabadilisha dhana ya mnyama wa kafara, jambo ambalo linaweza kubadilisha tafsiri ya kiitikadi na kifalsafa ya tendo hilo. Kwa mujibu wa Bassnett (2014), vipengele vya ibada na imani ni miongoni mwa vipengele vigumu zaidi kuhawilishwa kwa sababu vinafungamana kwa karibu na mifumo ya kiutamaduni.

Aidha, mabadiliko haya yanaweza kufasiriwa kwa kutumia dhana ya utotafsirikaji wa kitamaduni kama inavyoelezwa na Catford (1965), ambapo baadhi ya vipengele vya utamaduni haviwezi kuhamishwa kikamilifu kutokana na kukosekana kwa viwakilishi linganifu katika lugha lengwa. Hata hivyo, changamoto haipo tu katika kukosekana kwa visawe, bali pia katika maamuzi ya mfasiri yanayohusisha kubadilisha au kuacha vipengele fulani, jambo linalosababisha mwachano wa kidhima.

Kwa ujumla, mifano hii inaonyesha kuwa uhawilishaji wa dhana za kitamaduni katika tafsiri hii haukufanikisha kikamilifu ulinganifu wa kidhima, kwa kuwa baadhi ya dhana zimepotoshwa au kupunguzwa uzito wake wa kitamaduni. Hali hii inaathiri namna msomaji wa Kiswahili anavyopokea na kuelewa ujumbe, na hivyo kuthibitisha kuwa tafsiri ya vipengele vya utamaduni si uhamishaji wa moja kwa moja bali ni mchakato unaohitaji uangalifu mkubwa wa kisemantiki na kimuktadha.

Mabadiliko ya Taswira za Kitamaduni

Sehemu hii inachunguza namna taswira za kitamaduni zinavyobadilika katika tafsiri na athari za mabadiliko hayo kwa uwasilishaji wa maana na ujumbe. Taswira za kitamaduni hurejelea matumizi ya lugha ya picha—kama vile sitiari, nahau na vihisishi—ambavyo hubeba maana pana zinazofungamana na utamaduni fulani. Kwa mujibu wa Baker (2018), taswira hizi ni miongoni mwa vipengele vigumu zaidi kutafsiri kwa sababu maana yake haipo katika maneno pekee bali katika muktadha wa kitamaduni unaozizunguka.

Mfano wa kwanza unaonekana katika Data 3, ambapo kirai *"gates of heaven"* kimetafsiriwa kama *"milango ya ahera"*.

Data 3

MC: We drank ourselves silly. <u>Gates of heaven</u> were now open… (uk. 118)

MT: Tulilewa chakari. <u>Milango ya ahera</u> ilikuwa imetufungukia… (uk. 142)

Katika matini chanzi, kirai hiki kimetumika kwa njia ya kejeli kuashiria hali ya ulevi uliokithiri unaofanana na hali ya furaha au utepetevu uliopindukia. Hata hivyo, tafsiri ya *"ahera"* inaleta maana ya kidini inayohusishwa na maisha baada ya kifo, ambayo yanaweza kuwa ya hukumu au malipo. Mabadiliko haya yanabadilisha taswira kutoka katika muktadha wa ucheshi na kejeli hadi tafakari ya kiroho. Kwa mtazamo wa Nida (1964), hii ni ishara ya kushindwa kufanikisha ulinganifu wa kidhima kwa kuwa athari ya kihisia kwa msomaji wa Kiswahili inatofautiana na ile ya msomaji wa Kiingereza.

Mfano mwingine unaonekana katika Data 4, ambapo kihisishi *"Fuck you"* kimetafsiriwa kwa namna isiyoendana moja kwa moja na nguvu ya taswira ya asili.

Data 4

MC: …fading -white chalked walls with "F<u>uck you</u>" and other slogans (pg 127).

MT: Kuta chakavu za chaki, nyeupe zenye maandishi ya matusi kama "<u>nitajamiiana naye</u>" (Uk 152).

Katika utamaduni wa Kiingereza, kihisishi hiki hubeba hisia kali za hasira, dharau au uchokozi. Hata hivyo, tafsiri iliyotolewa inapunguza au kubadilisha nguvu ya taswira hii kwa kutumia lugha isiyo na ukali uleule au inayobadilisha mwelekeo wa kauli. Hali hii inaashiria kile anachokiita Newmark (1988) kupotea kwa "maana ya kihisia", (*expressive meaning*) ambapo nguvu ya kihisia ya matini chanzi haijadumishwa katika matini lengwa.

Mabadiliko haya ya taswira yanaweza pia kueleweka kwa kuzingatia hoja ya Bassnett (2014) kwamba tafsiri ya fasihi mara nyingi huhusisha uundaji upya wa picha za kitamaduni badala ya uhamishaji wake wa moja kwa moja. Hata hivyo, tatizo linatokea pale ambapo uundaji huu mpya unabadilisha kwa kiasi kikubwa maana na athari ya taswira husika. Katika mifano iliyojadiliwa, taswira za matini chanzi hazijahawilishwa ipasavyo bali zimebadilishwa, jambo linalosababisha mwachano wa kidhima.

Kwa ujumla, sehemu hii inaonyesha kuwa uhamishaji wa taswira za kitamaduni katika tafsiri hii haukufanikisha kudumisha athari na maana ya awali. Badala yake, taswira zimebadilika kwa namna inayopunguza au kubadilisha ujumbe, na hivyo kuathiri uzoefu wa msomaji wa lugha lengwa.

Uchujaji wa Utamaduni

Sehemu hii inachunguza namna mfasiri anavyochuja au anavyorekebisha vipengele vya utamaduni ili kuendana na matarajio, maadili na kanuni za lugha lengwa, na jinsi mchakato huo unavyozalisha mwachano wa maana na dhamira. Urekebishaji huu wa utamaduni (*cultural filtering*) mara nyingi hutokea pale ambapo vipengele vya matini chanzi vinaonekana kuwa visivyokubalika, visivyoeleweka au vyenye ukinzani na muktadha wa hadhira lengwa. Kwa mujibu wa Venuti (1995), mkabala huu unahusishwa na dhana ya uenyejishaji, ambapo matini hubadilishwa ili kuonekana ya kawaida na inayokubalika katika utamaduni lengwa.

Mfano dhahiri unaonekana katika Data 4, ambapo kihisishi *"Fuck you"* kimerekebishwa katika tafsiri kwa namna inayopunguza ukali wake wa moja kwa moja.

Data 4

MC: …fading -white chalked walls with "F<u>uck you</u>" and other slogans (pg 127).
MT: Kuta chakavu za chaki, nyeupe zenye maandishi ya matusi kama "<u>nitajamiiana naye</u>" (Uk 152).

Katika utamaduni wa Kiingereza, kauli hii hubeba hisia kali za hasira, dharau na uchokozi. Hata hivyo, kutokana na maadili ya lugha ya Kiswahili ambayo hupunguza matumizi ya matusi ya moja kwa moja hasa yahusuyo ngono, mfasiri amelazimika kutumia lugha iliyopunguzwa ukali au iliyozungukwa kwa tahadhari. Ingawa mkakati huu unalenga kulinda maadili ya hadhira lengwa, pia unasababisha kupungua kwa athari ya kihisia ya ujumbe. Kwa mtazamo wa Nida (1964), hatua hii inaathiri ulinganifu wa kidhima kwa kuwa msomaji wa Kiswahili hapati nguvu ileile ya kihisia iliyokusudiwa katika matini chanzi. Vilevile, Data 5 inaonyesha urekebishaji wa utamaduni kupitia upanuzi wa maana.

Data 5

MC: The <u>old man</u> too. Always remember your father and mother (pg 128).
MT: <u>Mzee wa kijiji</u> pia. Kila mara wakumbuke baba na mama yako (uk 153).

Neno *"old man"* limetafsiriwa kama *"mzee wa kijiji"*, jambo linaloongeza dhana ya mamlaka ya kijamii ambayo haipo katika matini chanzi. Katika muktadha wa Kiingereza, "old man" linaweza kurejelea mtu mzima mwenye umri mkubwa bila kumhusisha moja kwa moja na nafasi ya uongozi. Hata hivyo, katika Kiswahili, matumizi ya "mzee wa kijiji" yanaashiria nafasi maalum ya kijamii na kiutawala. Hii inaonyesha kuwa mfasiri amejaribu kuifanya dhana hiyo iwe na uzito unaoeleweka kwa hadhira ya Kiswahili, lakini kwa kufanya hivyo amebadilisha dhamira ya awali ya matini. Kama anavyoeleza Venuti (1995), uenyejishaji mara nyingi huondoa utofauti wa kitamaduni kwa kuifanya matini ionekane kama ya utamaduni lengwa, hali inayoweza kufifisha sifa za matini chanzi.

Aidha, mabadiliko haya yanaonyesha mvutano uliopo kati ya uelewekaji na uaminifu katika tafsiri. Newmark (1988) anaeleza kuwa tafsiri ya kimawasiliano hulenga uelewekaji kwa hadhira lengwa, hata kama itahitaji kubadilisha baadhi ya vipengele vya matini chanzi. Hata hivyo, katika fasihi, mabadiliko kama haya yanapaswa kufanywa kwa uangalifu ili kuepuka kubadilisha dhamira na mtazamo wa mwandishi.

Kwa ujumla, uchanganuzi huu unaonyesha kuwa urekebishaji wa utamaduni ni mkakati unaotumiwa kwa kiasi kikubwa katika tafsiri hii ili kuendana na maadili ya

Kiswahili. Hata hivyo, mkakati huu umechangia mwachano wa kidhima kwa kubadilisha nguvu ya kihisia na maana ya baadhi ya vipengele vya matini chanzi. Hali hii inaonyesha kuwa ingawa uenyejishaji unaweza kuboresha uelewekaji, pia unaweza kuathiri uhalisia na athari ya matini ya asili.

Athari kwa Msomaji wa Kiswahili

Sehemu hii inachunguza athari za mwachano wa kitamaduni kwa msomaji wa lugha lengwa, kwa kuangazia namna tafsiri inavyobadilisha uelewa na uzoefu wa matini. Kama inavyosisitizwa katika Nadharia ya Ulinganifu, hasa ule wa kidhima, mafanikio ya tafsiri hupimwa kwa kiwango ambacho msomaji wa lugha lengwa hupata athari inayolingana na ile ya msomaji wa matini chanzi (Nida, 1964). Hata hivyo, uchanganuzi uliotangulia umeonyesha kuwa katika visa vingi, athari hii haijadumishwa kikamilifu.

Kwanza, msomaji wa Kiswahili anapokea maana tofauti kutokana na mabadiliko ya dhana na taswira za kitamaduni. Pale ambapo dhana zimepotoshwa au kupunguzwa uzito wake—kama ilivyo katika tafsiri ya vipengele vya kijamii na kidini—msomaji hupata uelewa usioendana kikamilifu na ule uliokusudiwa katika matini chanzi. Kwa mujibu wa House (2015), hali hii husababisha kile kinachoitwa "kutolingana kwa kiuamilifu" (*functional mismatch*), ambapo matini tafsiriwa inashindwa kutekeleza dhima ileile ya mawasiliano kama matini chanzi.

Pili, msomaji anapokea utamaduni uliorekebishwa au uliobadilishwa. Kupitia mkakati wa uchujaji wa utamaduni, baadhi ya vipengele vya utamaduni wa chanzi hubadilishwa ili kuendana na maadili ya Kiswahili. Ingawa hatua hii huongeza uelewekaji, pia huondoa baadhi ya sifa bainifu za matini chanzi. Venuti (1995) anaonya kuwa hali hii inaweza kusababisha kufifia kwa utofauti wa kitamaduni kwa sababu matini huonekana kana kwamba ni zao la utamaduni lengwa badala ya kuwa tafsiri.

Tatu, katika baadhi ya matukio, msomaji hupokea utamaduni uliopunguzwa au usio kamili. Hii hutokea hasa pale ambapo vipengele vya kitamaduni vinaachwa bila kufafanuliwa au vinapotafsiriwa kwa njia isiyo kamili. Kama anavyoeleza Baker (2018), upungufu huu wa taarifa unaweza kuathiri uwezo wa msomaji kufasiri kwa kina maana ya matini na kuhusisha ujumbe wake na muktadha mpana wa kitamaduni.

Kwa kuzingatia hoja hizi, inaweza kusemwa kuwa tafsiri katika matini hii haijafanya kazi ya "kuvusha" utamaduni kwa ukamilifu, bali imeuhamisha kwa namna iliyobadilishwa. Kwa maneno mengine, tafsiri haibaki kuwa daraja la kuunganisha tamaduni mbili pekee, bali pia huwa chombo cha kuunda upya au hata kupunguza baadhi ya vipengele vya utamaduni wa chanzi. Hali hii inaathiri moja kwa moja uzoefu wa msomaji wa Kiswahili, ambaye hupokea matini yenye maana na athari tofauti kwa kiwango fulani na ile ya matini asilia.

Kwa ujumla, sehemu hii inaonyesha kuwa mwachano wa kitamaduni unaojitokeza katika tafsiri una athari kubwa kwa upokeaji wa matini. Inathibitisha hoja kuu ya makala hii kwamba tafsiri ya fasihi si uhamishaji wa utamaduni tu, bali ni mchakato unaoweza kuubadilisha au hata kuufuta kwa sehemu mguso wa utamaduni asilia.

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Hitimisho: Makala hii imechunguza uhawilishaji wa utamaduni na mwachano wake katika tafsiri ya fasihi kwa kutumia uchambuzi wa matini ya *Secret Lives and Other Stories* na tafsiri yake ya Kiswahili *Maisha ya Siri na Hadithi Nyingine*. Kwa ujumla, imebainika kuwa tafsiri ya fasihi haifanyiki katika kiwango cha kiisimu pekee bali pia katika kiwango cha kitamaduni, ambapo maana, taswira na dhamira hubadilishwa kulingana na muktadha wa lugha lengwa.

Uchambuzi umeonyesha kuwa vipengele mbalimbali vya utamaduni kama dhana za kijamii, taswira za kifasihi, marejeleo ya kiimani na vihisishi vya kihisia vimepitia mabadiliko tofauti katika mchakato wa tafsiri. Baadhi ya vipengele vimehawilishwa kwa ufanisi na kudumisha ulinganifu wa kidhima, ilhali vingine vimepoteza uzito wa kitamaduni au kubadilishwa kwa namna inayosababisha mwachano wa maana na athari ya ujumbe. Aidha, mbinu za uenyejishaji na uigenishaji pamoja na changamoto ya utotafsirikaji zimejitokeza kama vipengele muhimu vinavyoathiri uamuzi wa mfasiri.

Kwa msingi wa matokeo haya, utafiti umejibu swali lake kuu kwa kubainisha kuwa tafsiri ya *Maisha ya Siri na Hadithi Nyingine* haijadumisha kikamilifu ulinganifu wa kidhima katika vipengele vyote vya kitamaduni. Badala yake, kuna ushahidi wa mwachano wa kitamaduni unaotokana na maamuzi ya kimkakati ya tafsiri, tofauti za kiutamaduni, na ukosefu wa visawe sahihi katika baadhi ya mazingira.

Kwa hiyo, hitimisho kuu la makala hii ni kwamba tafsiri ya fasihi si uhamishaji wa maana pekee bali ni mchakato wa uundaji upya wa utamaduni, ambapo mtafsiri huunda upya matini chanzi kulingana na matarajio, maadili na mifumo ya utamaduni lengwa. Hii ina maana kuwa kila tafsiri hubeba kiwango fulani cha mabadiliko ya kitamaduni, iwe kwa kuimarisha au kupunguza mguso wa matini asilia.

Mapendekezo: Kwa kuzingatia matokeo ya utafiti huu, inapendekezwa kuwa watafsiri wazingatie kwa makini usawazishaji kati ya uaminifu kwa matini chanzi na uelewekaji kwa hadhira lengwa. Ili kupunguza upotevu wa maana za kitamaduni, wanapaswa kutumia mikakati ya tafsiri inayochanganya uenyejishaji na ugenishaji kulingana na muktadha wa kipengele kinachotafsiriwa. Aidha, ni muhimu wawe na uelewa mpana wa muktadha wa kitamaduni wa lugha chanzi na lugha lengwa ili kuepuka kupotosha dhana, taswira na vipengele vingine muhimu vya utamaduni.

Vilevile, watafiti wanahimizwa kuendelea kuchunguza kwa kina uhusiano kati ya tafsiri na utamaduni kwa kutumia matini mbalimbali za kifasihi badala ya kujikita katika hadithi fupi pekee. Pia, kuna haja ya kufanya tafiti linganishi zinazohusisha tafsiri tofauti za matini moja ili kubainisha namna mikakati mbalimbali ya tafsiri inavyoathiri uhawilishaji wa utamaduni na kiwango cha mwachano wa kitamaduni.

Kwa upande wa tafiti zijazo, inapendekezwa kufanyika kwa tafiti zinazochunguza athari za uhawilishaji wa utamaduni kwa wasomaji halisi (*reader-response studies*) ili kubaini namna mabadiliko ya kitamaduni katika tafsiri yanavyoathiri uelewa na upokeaji wa matini. Aidha, matumizi ya mbinu za kidijitali katika uchanganuzi wa tafsiri yanaweza kusaidia kubainisha kwa upana zaidi mifumo ya mwachano wa kitamaduni katika tafsiri za Kiswahili.

Hatimaye, kuna haja ya kufanya tafiti zinazochunguza nafasi ya mtafsiri kama msuluhishi wa kitamaduni katika mazingira ya lugha za Kiafrika ili kuongeza uelewa kuhusu mchango wake katika kuhifadhi na kuhawilisha utamaduni kupitia tafsiri ya fasihi.

MAREJELEO

Baker, M. (2018). *In other words: A coursebook on translation* (3rd ed.). Routledge.
Bandia, P. (2008). *Translation as reparation: Writing and translation in postcolonial Africa*. St. Jerome Publishing.
Bassnett, S. (2014). *Translation studies* (4th ed.). Routledge.
Catford, J. C. (1965). *A linguistic theory of translation*. Oxford University Press.
Creswell, J. W. (2014). *Research design: Qualitative, quantitative, and mixed methods approaches* (4th ed.). Sage.
House, J. (2015). *Translation quality assessment: Past and present*. Routledge.
Lefevere, A. (1992). *Translation, rewriting, and the manipulation of literary fame*. Routledge.
Munday, J. (2016). *Introducing translation studies: Theories and applications* (4th ed.). Routledge.
Newmark, P. (1988). *A textbook of translation*. Prentice Hall.
Nida, E. A. (1964). *Toward a science of translating*. E. J. Brill.
Patton, M. Q. (2002). *Qualitative research and evaluation methods* (3rd ed.). Sage.
Venuti, L. (1995). *The translator's invisibility: A history of translation*. Routledge.